# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA TANO

**02 FEBRUARI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA TANO – TAREHE 02 FEBRUARI, 2026

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kuhusu Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda mrefu 2026/27 - 2050/51, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/27 - 2028/29.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda mrefu 2026/27 - 2050/51, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31), Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/27 - 2028/29..

## III. MASWALI:

## OFISI WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**69. MHESHIMIWA ESTER AMOS BULAYA (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Mradi wa TACTIC Awamu ya Tatu utaanza kutekelezwa katika Jimbo la Bunda Mjini.

**70. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya Masama pamoja na nyumba za Watumishi wa Kituo hicho.

**71. MHESHIMIWA BENJAMIN LUKUBHA NGAYIWA (KAHAMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuipandisha hadhi Hospitali ya Manispaa ya Kahama kuwa Hospitali ya Rufaa.

**72. MHESHIMIWA PASCHAL INYASI CHINYELE (DODOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Wananchi Kata ya Mbalawala wamezuiwa kuendeleza ardhi wanayomiliki kwa maelezo kuwa ni sehemu ya Bonde la Kati Singida.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**73. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, nini hatma ya Mradi wa TASAF nchini.

## WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

**74. MHESHIMIWA ENG. FADHILI SANDALI CHILOMBE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Mnara wa Mawasiliano katika Vijiji vya Kazamoyo, Imani na Kilimani - Jimbo la Tunduru Kusini.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**75. MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MTAMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanza upembuzi wa ujenzi wa Reli ya SGR kutoka Dar es Salaam hadi Kusini kufuatia maandalizi ya Mradi wa LNG.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**76. MHESHIMIWA SAID IBRAHIM MZIMBA (MTAMBILE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itatenga Bajeti ya ukarabati wa Vituo vya Polisi Mtambile na Kengeja kwa kuwa vimechakaa.

**WIZARA YA MAJI:**

**77. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (ITWANGI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Vijiji 18 vya Tinde *package*.

**78. MHESHIMIWA ISACK JOSEPH COPRIANO (MONDULI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha Mradi wa Maji wa Vijiji 13 vya Jimbo la Monduli.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**79. MHESHIMIWA JOHN JOHN NCHIMBI (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha kukoboa Kahawa Nyasa kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais.

**WIZARA YA UJENZI:**

**80. MHESHIMIWA JANETH PETER PINDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Barabara kutoka Wilaya ya Tanganyika hadi Uvinza.

**81. MHESHIMIWA ENG. AMOSY WILLIAM MAGANGA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Ipole - Rungwa na Sikonge - Kipili kwa kiwango cha lami.

**82. MHESHIMIWA CHARLES MHANDO NJAMA (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Iini Barabara ya Old Korogwe - Kwamndolwa km 10 itajengwa kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA KILIMO:**

**83. MHESHIMIWA YOHANA STEPHEN MSITA (ITIGI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kupandisha bei ya zao la Dengu baada ya bei kuporomoka.

**84. MHESHIMIWA SHAFFIN AHMEDALI SUMAR (UYUI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali inawasaidiaje Wakulima wa Tumbaku kupitia AMCOS kulipwa fedha jumla ya Dola Milioni 1.2 wanazodai kwenye Makampuni.

**85. MHESHIMIWA ALAN THOMAS MVANO (KAKONKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wakulima wa Zao la Muhogo Kakonko wanapata Soko la Uhakika.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**86. MHESHIMIWA MUSA GODFREY MBUGA (KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mbinu gani mpya za kukabiliana na Tembo Vijiji vya Ng'hanga, Mwambongo, Matale, Longalonhinga, Sakata, Nyanza, na Banhya.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**87. MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha Wanawake Wajasiriamali wanashiriki moja kwa moja kwenye utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**88. MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (KARAGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha VETA Tarafa za Nyabiyonza na Nyakakika kwani kuna umbali mrefu toka Chuo cha VETA Kayanga.

**IV. KAMATI YA MIPANGO:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda

mrefu 2026/27 - 2050/51, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/27 - 2028/29.

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**02 FEBRUARI, 2026** **KATIBU WA BUNGE**